# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 NOVEMBA, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2026

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE TAREHE 11-20 NOVEMBA, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhohofika. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuendelea kubaki kusini, na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, kati, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kusini mwa nchi. Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) lilikuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonecia). Hali hii iliimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale yaliyoko nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2026

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, Magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na maeneo ya kusini mwa nchi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kusini na pwani ya Kaskazini.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2026

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuendelea kubaki kusini, na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya jirani. Vilevile,

joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonecia). Hali hii inatarajiwa kuimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale yaliyoko nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

**2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 NOVEMBA, 2026**

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua zinazoambatana na ngururumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngururumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***